



MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MFUMO SHIRIKISHI WA UHAKIKI (PGS)

Umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ulioandaliwa na TOAM kwa kushirikiana na wadau wa PGS Tanzania



MAANDALIZI YA MAARIFA HAYA

- Nakala hii ni tafsiri ya kiswahili ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) uliotengenezwa awali kwa lugha ya Kiingereza kupitia ushirikiano wa shirika la kilimohai Tanzania (TOAM) na IFOAM – Organics International.
- Mwongozo huo ulishirikisha wadau wa PGS nchini Tanzania kuchangia ujuzi na maarifa ya namna mfumo huu unapaswa kutekelezwa.
- Kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (KHEA), TOAM iliweza kutafsiri mwongozo wa mafunzo haya kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa wadau mbali mbali wa mnyororo wa thamani. iliunga mkono tafsiri ya mwongozo huu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, kama sehemu ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa maarifa kuhusu PGS.

UTANGULIZI KUHUSU MAARIFA HAYA

- Mwongozo huu wa Mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ni sehemu ya mfululizo wa nyenzo za mafunzo unaojumuisha moduli tano, zilizolenga kuwajengea washiriki uelewa na uwezo wa kutumia Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) katika Kilimohai.
- Nakala hii imejikita katika moduli 2 na inatoa maudhui kuhusu vipengele vya msingi vinavyounda PGS, sifa za PGS imara, na jinsi ya kushughulika na ukiukaji wa viwango baina ya wana PGS.
- Nakala nyingine za mafunzo kwa ajili ya moduli zinazofuata zinapatikana kama sehemu ya mfululizo huu, hivyo watumiaji wanashauriwa kuzitumia kwa pamoja ili kupata maudhui kamili ya mafunzo ya PGS.

MODULI YA PILI

VIPENGELE GANI VINAUUNDA MFUMO SHIRIKISHI WA UHAKIKI (PGS)?

Muhimu: Seti hii ya slides za mafunzo kwa moduli ya 1-5 inapaswa kutumika kwa kufuata mwongozo wa Mtaala wa Mafunzo ya PGS kwa Wawezeshaji (ToT), 2025

2.1 Vipengele vinavyounda mfumo wa PGS

Yaliyomo:

- Malengo ya kujifunza
- Kuelewa vipengele vya mfumo wa PGS
- Zoezi la 1: Kutambua sifa na shughuli za vikundi vya PGS zinazoakisi vipengele vya PGS



2.1 Vipengele vya Mfumo wa PGS


Lengo la Kujifunza



Mwisho wa mada hii, washiriki wataweza:
Kuelewa vipengele vya msingi vya mfumo wa PGS
na kuvitumia katika shughuli za vikundi vyao vya
PGS.

Vipengele vya PGS

PGS ni nini– Maana & vipengele



Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS):

- Ni Mfumo wa uhakiki wa ubora wa Kilimohai unaofanyika ngazi ya jamii.
- Mfumo huu unaotegemea ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhakiki wa wakulima.
- Unaojengwa juu ya uaminifu, ushirikiano wa kijamii na kubadilishana maarifa.

Kipengele cha 1: Dira ya Pamoja

- Ndio msingi unao waunganisha wadau wote wa PGS.
- Taswira ya pamoja ya hali inayotarajiwa kufikiwa siku zijazo na ambayo huongoza shughuli za kikundi.
- Lazima ibadilishwe kuwa hatua za vitendo zinazoweza kutekelezwa.



Mfano: Wakulima wote wanakubaliana kuzalisha mazao kwa kuzingatia kanuni za Kilimohai na kuuza kwa kutumia alama ya Kilimohai

Kipengeele cha 2: Ushiriki

- Ushiriki kamilifu wa wadau wa msingi katika shughuli za PGS.
- Wajibu na maamuzi hugawanywa kwa pamoja.
- Ushiriki huimarisha utekelezaji wa dira, malengo na shughuli za kikundi.



Mfano: Wanachama hushiriki katika ukaguzi wa mashamba, mikutano na maamuzi ya kikundi.

Kipengeele cha 3: Uwazi

- Taratibu na maamuzi yote yanafanyika kwa uwazi.
- Huhimiza ushiriki wa wadau wote wanahusishwa katika kila hatua.
- Hutoa fursa sawa ya kupata taarifa kwa wanachama wote.



Mfano: Ripoti za ukaguzi na maamuzi ya kikundi zinapatikana kwa wanachama wote.

Kipengele cha 4 : Uaminifu

- Wanachama wanatenda kwa uadilifu.
- Husaidia kujenga imani baina ya wakulima na walaji
- Huimarisha sifa ya kuaminika kupitia vitendo na mawasiliano



Mfano: Mkulima hutoa taarifa sahihi kuhusu shughuli zote za uzalishaji shambani.

Kipengeele cha 5 : Uwiano

- Wanachama wote wana haki na wajibu sawa.
- Ushiriki wa wanawake, vijana na makundi mengine huzingatiwa.
- Wadau wote kufanya kazi pamoja kuelekea utekelezaji wa dira na malengo ya PGS.



Mfano: Wanawake na wanaume wanashiriki katika kamati na maamuzi ya PGS.

Kipengele cha 6 : Mchakato endelevu wa kujifunza



Wadau wote
wanaelewa
viwango na
kanauni za PGS



Mbinu zinazokubalika
na hatua za
kushughulikia ukiukwaji
zimeainishwa wazi



Huchangia
kufanikisha
malengo ya
msingi ya PGS

Mfano: Wakulima hujifunza kupitia mashamba darasa, mafunzo na ziara za kujifunza.

Zoezi la 1: Tathimini mfumo wenu wa PGS.

Mfano:

Swali	Ndiyo	Hapana
Tuna viwango vilivyoandikwa?	☐	☐
Tuna mfumo wa ukaguzi?	☐	☐
Tunatunza kumbukumbu?	☐	☐
Tuna utaratibu wa kutoa adhabu?	☐	☐
Tunatumia nembo ya PGS?	☐	☐

Nini kinaenda vizuri?
Changamoto?
Namna ya kuboresha?



Muda: Saa 1

2.2 Sifa za mfumo Imara wa PGS

2.2 Sifa za Mfumo Imara wa PGS

Yaliyomo

- Malengo ya kujifunza
- Sifa kuu za mfumo wa PGS
- Zoezi la 2: Chambua mifumo ya PGS na washiriki



Lengo la kujifunza:

Kuwawezesha washiriki kuelewa sifa muhimu za mfumo wa PGS na jinsi zinavyochangia utendaji wake.



Na. Sifa za msingi za PGS

- 1 Kuna kanuni na taratibu zilizoandaliwa na kukubaliwa na wadau.
- 2 Kuna mfumo unaoanzishwa na kuendeshwa na jamii ya wakulima wenyewe.
- 3 Unafaa kwa wakulima wadogo
- 4 Unazingatia kanuni na maadili ya Kilimohai
- 5 Una kumbukumbu na taratibu zilizoandikwa


Na. Sifa za msingi za PGS

- | | |
|----|--|
| 6 | Una mfumo wa kuhakiki uzingatiaji wa viwango |
| 7 | Una mipango ya kuwawezesha wakulima |
| 8 | Una nyaraka za makubaliano kati ya wadau |
| 9 | Unatumia nembo au alama ya utambulisho |
| 10 | Una hatua zilizoainishwa za kushughulikia ukiukwaji wa viwango |

Vipengele na sifa za PGS

Vipengele vyote vya PGS vinalenga kuhakikisha na kuimarisha uadilifu wa Kilimohai.

Mchakato wa PGS



Zoezi 2:

Maswali ya Majadiliano

1. Ni sifa zipi tayari zipo katika kikundi chenu?
2. Ni sifa zipi bado hazijaimarika?
3. Ni hatua gani zinahitajika ili kuimarisha mfumo wa PGS?

**Maswali ya majadiliano
katika vikundi**



Muda: Dakika 30–45

2.3 Jinsi ya Kushughulika na Ukiukwaji wa Viwango katika PGS



Ukiukwaji wa Viwango ni Nini?

- Kutofuata kanuni, viwango au taratibu za PGS zilizowekwa.
- Ukiukwaji unaweza kutokea kwa bahati mbaya au kwa makusudi.



Kanuni za Kuzingatia Wakati wa Kuamua adhabu kwa wakiukaji wa taratibu

Kanuni	Maelezo
Zinaweza Kutekelezeka	Adhabu au hatua zinazotolewa ziwe halisi na zinazoweza kutekelezwa.
Zinakubalika	Adhabu ziwe zimekubaliwa na wanachama wa PGS.
Uwazi	Taratibu za kutoa adhabu ziwe wazi na zitekelezwe kwa haki.
Kumbukumbu	Maamuzi yote yahifadhiwe katika kumbukumbu na yaweze kufuatiliwa.
Usawa	Wanachama wote watendewe sawa bila upendeleo.

Mifano ya Ukiukwaji wa Viwango

Makosa madogo

Kutowasilisha kumbukumbu za msimu wa uzalishaji kwa wakati.

Makosa makubwa

Matumizi ya kemikali zilizopigwa marufuku.

- Uchafuzi wa mazao au shamba kwa vitu visivyoruhusiwa.
- Kuchanganya mazao yaliyohakikiwa na yasiyohakikiwa.
- Kuuza kama bidhaa za Kilimohai mazao yaliyotoka nje ya maeneo yaliyohakikiwa.



Jinsi ya Kushughulikia Ukiukwaji wa viwango

Hatua au adhabu zinazotolewa zinapaswa kuwa:

- **Zinazoendana** na ukubwa wa kosa – adhabu izingatia uzito wa kosa lililofanyika.
- Zilikubaliwa **mapema** – ziwe zimejadiliwa na kukubaliwa na wanachama wa PGS.
- Zimeandikwa na kuhifadhiwa – taarifa na maamuzi yawe katika **kumbukumbu zinazoweza kufikiwa**.
- Zinaweza kukatiwa **rufaa** – mwanachama apewe haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi uliotolewa.

Mifano ya Adhabu kwa Ukiukwaji wa Viwango katika PGS

Hali inayoweza kujitokeza kwenye PGS	Mfano wa Adhabu inayoweza kutolewa
Kutohudhuria siku ya ukaguzi au shughuli muhimu ya kikundi bila sababu ya msingi	Kumbusho au onyo
Ukiukwaji mdogo wa viwango (mfano: kutohifadhi kumbukumbu muhimu)	Onyo au maelekezo ya kurekebisha kasoro
Kurudia ukiukwaji mdogo mara kwa mara	Onyo kali na kusimamishwa kwa muda hadi hatua za marekebisho zikamilike
Ukiukwaji mkubwa wa viwango (mfano: matumizi ya pembejeo zilizopigwa marufuku)	Kusimamishwa au kuondolewa katika mfumo wa PGS na kufutiwa uthibitisho
Udanganyifu uliothibitishwa	Kuondolewa katika mfumo wa PGS na kufutiwa uthibitisho; anaweza kuzuiwa kurejea kwa muda au moja kwa moja

Zoezi la 4: Tengenezeni mifano mingine ya ukiukwaji wa viwango na adhabu zinazoweza kutolewa katika mazingira yenu.

Muda: Dakika 30

Nembo ya kilimohai

- Nembo ya Kilimohai ya Afrika Mashariki (EAOM) hutumika kutambulisha bidhaa za Kilimohai katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Hufuata viwango vya kilimohai Afrika Mashariki na vinavyolingana



Nembo nyingine zinazotumiwa na PGS mbalimbali duniani



HITIMISHO

- Moduli hii imeangazia vipengele sita vya msingi vya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) vinavyoweza mfumo kufanya kazi kwa ushirikiano, uwazi, uaminifu na usawa. Vipengele hivi vinaweka msingi wa namna wanachama wa PGS wanavyoshirikiana katika kuhakikisha uadilifu na ubora wa mfumo.
- Katika Moduli ya 3 utajifunza zaidi kuhusu hatua za kuanzisha PGS na namna ya kusimamia mfumo huo ili kudhibiti ubora wa bidhaa zinazozalishwa kwa kilimohai

*Imeandaliwa na Shirika Mwamvuli la Kilimohai Tanzania
(TOAM) kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki
(Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology
Tanzania - KHEA)*

Kupata moduli nyingine tembelea jukwaa la kidijitali la maarifa ya
kilimohai na kilimoikolojia katika tovuti: <https://khea-africa.org/>

Tunapatikana:

Mtaa wa Samora Avenue, Jengo la Kelvin House, gorofa ya Kwanza.
Kwa mawasiliano Zaidi tupigie kupitia +25574413499